# MASWALI YA MARUDIO ~2026

# MAANDALIZI YA KCSE: MATUMIZI YA LUGHA KARATASI YA PILI


## 0713452040

## 0724289534

## EDWIN ODERO


## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

**Karatasi ya pili** ni karatasi ya lugha. Katika mtihani wa kitaifa, karatasi ya pili **(102/2)**, huhusisha kitengo cha **ufahamu, ufupisho, sarufi** na **matumizi ya lugha** na **isimujamii.** Huu ndio utaratibu na mpangilio ambao umerejelewa kwa kina katika karatis hii.

**A. UFAHAMU** ~ **(alama15)**
**B. UFUPISHO** ~ **(alama15)**
**C. MATUMIZI YA LUGHA** ~ **(alama40)**
**D. ISIMUJAMII** ~ **(alama10)**

**MWANAFUNZI**

**1. Ili kufaulu katika karatasi ya pili:**
- Jipime kwa mazoezi; kwenye vikundi au kibinafsi kwa mtihani wako.
- Fanya mazoezi jinsi hali ya mtihani huwa huku ukizingatia muda halisi ~ muda wa saa:$2\frac{1}{2}$
- Jisahihishe kwa uaminifu. Iwapo umekosa, kubali umekosa.
- Wakati unajisahihishia, chambua makosa yako kwa mujibu wa yale majibu.
- Fanyia kazi udhaifu wako kwa kutambua mada zilizokupa changamoto
- Shughulikia mada hizo kabla ya karatasi nyingine.

**2.** Maisha yako ni kama penseli. Penseli haiwezi ikaandika lolote hadi pale itakuwa mikononi mwa mtu. Iwapo unataka kuacha alama nzuri katika maisha yako, lazima ukubali kushikwa mkono na kuongozwa. Kubali kushikwa mkono na walimu wako wana busara.

**3.** Epuka uzembe na imani potovu ~ carelessness and negative attitude

**4.** Kushindwa sio kinyume cha ufanisi, ni mojawapo ya hatua katika mchakato wa ufanisi. Kukosa pia ni ishara kuwa unajaribu. Usife moyo. Usikate tamaa. Iwapo utajiamini, una uwezo wa kufanikisha ndoto zako.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA KUJIBU MASWALI

**1. Maagizo**
- Chukua dakika **tano** katika sehemu hii kusoma na kuelewa maagizo
- Muhimu zaidi fuata maagizo uliyosoma.

**Tanbihi: ~ Soma, elewa kisha fuata.**

## 2. Muda

- Maagizo ~ **dakika 5**
- Ufahamu **~ dakika 30 ~(alama15)**
- Ufupisho **~ dakika 30 ~(alama15)**
- Lugha ~ **dakika 60 ~(alama40)**
- Isimujamii ~ **dakika 20 ~(alama10)**
- Dakika **5** ~ **kupitia majibu yako na kurekebisha makosa yaliyomo.**

**Tanbihi:**

- Hakikisha umetumia muda wako vyema ili upate nafasi ya kuyahariri majibu yako yote. Huenda ukawa na hoja za kuongezea hapa na pale na kurekebisha makosa ambayo pengine ulifanya ukijibu.

## 3. Kaida za maswali

- Anza kwa matumizi ya lugha mara moja bila kufikiria chochote. Akili ingali nathari ~sehemu hii ina **alama40**
- Karatasi hii inaitwa karatasi ya lugha, kwa hivyo ni sharti ufuate zile sheria za lugha; ufahamu, ufupisho, sehemu zote.
- Jibu maswali yote kulingana maagizo.
- Uwasilishaji mzuri wa kazi ni muhimu. Kazi yako iweze kusomeka vizuri. Tumia hati nadhifu. Usifutefute maandishi na kuifanya kazi kuwa chafu.
- Jibu lilenge tu mahitaji ya swali, usitumie maneno mengi yasiyo na maana
- Zingatia ***vijisehemu*** vya swali bila uzembe. Baadhi ya maswali huwa na sehemu zaidi ya moja.
- Zitumie vyema kurasa za kijitabu cha majibu huku ukiepuka kufutafuta sana kazi yako. Kufuta kwingi kuna maana ya kubabaika, kukosa umakinifu, kunakili kazi ya mwengine au kukosa uhakika wa kile unachokifanya.

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K6

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya I – i **(alama1)**

**(b)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa matawi: **(alama4)**

Mkulima mzembe amepata hasara.

**(c)** Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimchezea. **(alama3)**

**(d)** Taja sauti mbili zinazotamkiwa midomoni **(alama3)**

**(e)** Kanusha sentensi ifuatayo: **(alama2**)

Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba.

**(f)** Kitenzi **fumbata** kiko katika hali(kauli) ya………… **(alama1)**

**(g)** Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha:

**(i)**Wakati **(alama1)**

**(ii)**Mahali **(alama1)**

**(h)** Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa **(alama2)**

**(i)** Mhunzi mrefu alishinda tuzo

(Anza kwa: Tunzo…)

**(ii)** Mwanafunzi huyu anasoma Kifaransa.

(Anza kwa: kiashiria kisisitizi…)

**(i)** Sentensi hizi ni za aina gani?

**(i)**Lonare anatembea kwa kasi **(alama1)**

**(ii)**Halima anaandika ilhali Enkomwa anasoma. **(alama1)**

**(j)** Tunga sentensi moja ukitumia neno 'seuze' **(alama1)**

**(k)** Bainisha kirai nomino na kirai tenzi katika sentensi: **(alama2)**

Jirani mwema alinipa chakula.

**(l)** Unda nomino kutokana na vitenzi:

**(i)**Chelewa **(alama1)**

**(ii)**Andika **(alama1)**

**(m)** Onyesha hali katika sentensi zifuatazo

**(i)** Huenda mvua ikanyesha leo. **(alama1)**

**(ii)** Miti hukatwa kila siku duniani. **(alama1)**

**(n)** Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neno 'japo' **(alama1)**

**(i)**Selina alijitahidi sana.

**(ii)**Selina hakushinda mbio hizo.

**(o)** Andika kinyume cha: **(alama2)**

Mwise alikunja nguo alizokuwa ameanika.

**(p)** Sahihisha sentensi: **(alama1)**

Mtoto ambaye niliyemsomesha ameasi jamii.

**(q)** Andika katika msemo wa taarifa **(alama2)**

"Sitathubutu kumpa pesa zangu." Mkolwe alisema.

**(r)** Tunga sentensi kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo: **(alama2)**

Suka na zuka

**(s)** Eleza matumizi ya ritifaa katika: N'shamchukua. **(alama2)**

**(t)** Andika udogo na ukubwa wa neno 'kiti' **(alama2)**

**(u)** Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi: **(alama2)**

Sofia na Raeli wanaandaliwa chai na mpishi

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K7

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania **(alama2)**

**(b)** Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Nzovu na Bi. Makambo.

Watoto hawa wote ni wa Bwana na Bi. Makambo.

**(c)** Unda nomino moja kutokana na kitenzi "ghalifika" **(alama1)**

**(d)** Andika kwa wingi: Nyundo hii imevunjika mpini wake **(alama1)**

**(e)** Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia jedwali. **(alama3)**
Mvulana mrefu anavuka barabara

**(f)** Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo **(alama2)**

**(i)** Karama

**(ii)** Gharama

**(g)** Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Mtoto mwenyewe alienda shambani.

**(ii)** Kazi yetu haihitajiki shuleni.

**(h)** Koloni au nukta mbili (:) hutumiwa katika kuorodhesha. Onyesha matumizi mengine matatu ya koloni (:) **(alama3)**

**(i)** Tunga sentensi itakayoonyesha, matumizi ya kihusishi cha a - unganifu. **(alama2)**

**(j)** Bainisha kishazi hutu na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri.

**(k)** Ainisha viambishi katika neno: kujidhiki **(alama2)**

**(l)** Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.

**(m)** Andika viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Chakula

**(ii)** Kwetu

**(n)** Badilisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali ya kuamuru **(alama2)**

Baba ingia ndani

**(o)** Eleza maana ya sentensi **(alama2)**

"Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba na ningalistarehe."

**(p)** Fafanua aina za hali zinazozotumika katika sentensi hizi **(alama2)**

**(i)** Mwimbaji aliimba, akacheka na akachangamsha sana.

**(ii)** Shangazi huja kila siku

**(q)** Tunga sentensi moja itakayoonyesha maana mbili tofauti za neno **pembe** **(alama2)**

**(r)** Andika katika msemo wa taarifa: **(alama3)**

Nitakuarifu nikimwona." Elma alisema.

**(s)** Nyambua kitenzi "ota" kama kinavyotokea katika kirai "ota ndoto" ili tofauti tatu zijitokeze **(alama3)**

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K8

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2025 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tambua mzizi katika neno: msahaulifu **(alama1)**

**(b)** Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha nomino **(alama1)**

**(c)** Andika kinyume cha: **(alama2)**

Wasichana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

**(d)** **(i)** Fafanua maana ya "mofimu huru" **(alama1)**

**(ii)**Toa mfano mmoja wa mofimu huru **(alama1)**

**(e)** Tambua kiambishi **awali** na kiambishi **tamati** katika neno: **(alama2)**

alaye

**(f)** Tumia kirejeshi amba- kuunganisha sentensi zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Mwanafunzi yule ni mrefu

**(ii)** Mwanafunzi amepita mtihani

**(g)** Sahihisha sentensi hii: Waya yangu imepotea **(alama1)**

**(h)** Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo **(alama1)**

Mpishi ammpikia mgeni wali vizuri

**(i)** Neno 'chuo' lina maana ya 'Shule inayotoa mafunzo maalum ya kazi fulani'

Tunga sentensi mbili kubainisha matumizi mengine mawili ya neno hili **(alama2)**

**(j)** Ibadilishe chagizo ya mahali kuwa ile ya wakati katika sentensi ifuatayo (alama

Mchezaji aliucheza mpira mjini Malindi.

**(k)** Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Yohana alimpigia Husha mpira

**(l)** Kanusha:

Sisi tumemaliza kujenga nyumba ambayo ingalikuwa yake angalifurahia. **(alama2)**

**(m)** Unda nomino kutokana na:

**(i)** Zingua **(alama1)**

**(ii)** Tosa **(alama1)**

**(n)** Ichoree vielelezo matawi ya sentensi: **(alama4)**

Paka mdogo amepanda mchungwani.

**(o)** Tumia kihusishi badilia kutunga upya sentensi hii: **(alama1)**

Mgeni yuko katika nyumba.

**(p)** Unda kitenzi kutokana na neno "sahili" **(alama1)**

**(q)** Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ **(alama2)**

**(r)** Tambua aina ya vitenzi kilichopigiwa mstari **(alama1)**

Mzee huenda anacheza kamari.

**(s)** Badilisha kiwakilishi kimilikishi kionyeshi kuwa kiwakilishi kionyeshi **(alama1)**

Chake kilipatikana chini.

**(t)** Tumia mfano mmoja mmoja kutofautisha baina ya sentensi sahili na sentensi ambatano **(alama4)**

**(u)** Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha nomino **(alama1)**

**(v)** Andika wingi: Mvua imebomoa nyumba ya jirani **(alama1)**

**(w)** Akifisha kifungu kifuatacho: **(alama4)**

huenda serikali iwazie kuidhibiti bei ya petroli hatuwezi kuyaruhusu makampuni ya petroli kuunyanyasa umma alisema waziri wa kawi ya petroli imeongezwa mara nne katika kipindi cha mwezi moja.

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K9

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika sentensi mbili zifuatazo kama sentensi moja kwa kutumia kiwakilishi kirejeshi. **(alama2)**

Duka la bahati lina bidha nyingi.

Juma anafanya kazi katika duka la bahati.

**(b)** **(i)** Eleza matumizi mawili ya kiambishi 'ji' **(alama2)**

**(ii)** Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi hayo **(alama2)**

**(c)** Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo **(alama2)**

<u>Ukuta</u> umemwumiza <u>mvulana</u> alipokuwa <u>akiuparaga.</u>

**(d)** Chora vielelezo matawi vya sentensi ifuatayo: **(alama4)**

Bakari, Rhoda na Hirsi wamefurahi kupita mtihani.

**(e)** Tambua sauti ambazo si za ufizi katika sauti hizi: **(alama1)**

/m/, /t/, /n/, /z/, /gh/

**(f)** Tunga sentensi sahihi ukitumia -fa- katika hali ya mazoea **(alama2)**

**(g)** Onyesha kwa kupiga mstari iliko shadda katika maneno mawili yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Malaika

**(ii)** Nge

**(h)** Eleza maana mbili za sentensi: **(alama2)**

Kiharusi chake kimewatia hofu.

**(i)** Tunga sentensi ukitumia kielezi cha jinsi cha nomino ifuatayo: Uganda **(alama2)**

**(j)** Bainisha sentensi sahili ziliizo katika sentensi mseto ifuatayo: **(alama3)**

Hamali ambaye ameugua alisema kuwa angekwenda hospitali jana.

**(k)** Andika ukubwa wa sentensi: Ndovu wa Kiafrika ameharibu kichaka. **(alama2)**

**(l)** Iandike tena sentensi bila kutumia vitenzi visaidizi **(alama2)**

Wachezaji huenda wakawa wanaweza kushinda mchezo wa leo.

**(m)** Andika kwa msemo halisi. **(alama3)**

Baba alipotuuliza kama tungependa kwenda Mombasa wakati wa likizo. Tulimjibu kwamba tulitaka kwenda Kisumu kwa kuwa tulikuwa hatujaliona Ziwa Victoria.

**(n)** Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota (*) katika sarufi ya Kiswahili **(alama3)**

**(o)** Kanusha sentensi ifuatayo: **(alama1)**

Hapo napo ndipo nitakapo

**(p)** Andika kinyume cha: **(alama1)**

Furaha amehamia mjini.

**(q)** Andika maneno yafuatayo katika kauli zilizoonyeshwa katika mabano (alama2)

| **Neno** | **kauli** | **jibu** |
|---|---|---|
| **(i)** Imba | (tendesha) | |
| **(ii)** Choka | (tendea) | |

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K10

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya irabu pekee **(alama1)**

**(b)** Eleza maana mbili za neno: barabara **(alama2)**

**(c)** Sahihisha sentensi **(alama1)**

Abiria walisafiri na ndege

**(d)** Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi: **(alama4)**

Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni.

**(e)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi: **(alama2)**

Usingeacha masomo, usingetaabika vile.

**(f)** Tunga sentensi ukitumia kielezi: **(alama2)**

**(i)** Idadi jumala

**(ii)** Namna linganisho

**(g)** Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi: **(alama2)**

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo.

**(h)** Eleza maana mbili zinazopatikana katika sentensi hii **(alama2)**

Neenda ukaniletee mbuzi

**(i)** Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli ya U–U **(alama2)**

**(j)** Andika katika usemi wa taarifa. **(alama3)**
"Mito yetu imechafuka sana; itabidi tuungane mikono wakubwa kwa wadogo, waume kwa wanawake ili tuisafishe." Mwanamazingira alituhimiza.

**(k)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama4)**

Amina na Mustafa huimba taarabu.

**(l)** Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Sikumwelewa alivyoeleza namna ya kuwatunza mbwa wake.

**(m)** Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi <u>la</u> katika kauli ya kutendwa **(alama2)**

**(n)** Eleza kazi ya kila kitenzi katika sentensi **(alama4)**

Mkulima angetaka kupalilia shamba lake mapema.

**(o)** Taja na kutofautisha vipasuo vya ufizi **(alama4)**

**(p)** Onyesha jinsi moja moja ya matumizi ya viwakifishi vifuatavyo **(alama3)**

**(i)** Nusu koloni (;)

**(ii)** Herufu kubwa

**(iii)** Kishangao (!)

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K11

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tumia mzizi '-enye" katika sentensi kama: **(alama2)**

**(i)** Kivumishi

**(ii)** Kiwakilishi

**(b)** Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa: **(alama2)**

Paka mweupe amenaswa mguuni.

**(c)** Taja vitamkwa vyenye sifa zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Kiyeyusho

**(ii)** Kimadende

**(d)** Onyesha shamirisho kitondo, shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari.

**(e)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali **(alama4)**

Maria anapika taratibu huku mama akimwelekeza vizuri.

**(f)** Nomino furaha iko katika ngeli gani? **(alama1)**

**(g)** Andika kinyume cha sentensi: **(alama2)**

Watoto wameombwa waanike nguo.

**(h)** Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa **(alama2)**

Mama alishangilia arusi ya mwana.

(Anza kwa: Mwana…)

**(i)** Tumia kirejeshi 'o' katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe.

**(j)** Kanusha sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyumbani.

**(k)** Ainisha vihusishi katika sentensi: **(alama2)**

Ame aliwasili mapema kuliko wengine halafu akaondoka

**(l)** Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno "chuma" **(alama1)**

**(m)** Unda nomino kutokana na kitenzi "tafakari" **(alama2)**

**(n)** Eleza maana mbili za sentensi: **(alama2)**

Tuliitwa na Juma

**(o)** Ainisha viambishi katika kitenzi: tutaonana **(alama2)**

**(p)** Tunga sentensi moja ukitumia kiungansihi cha kinyume **(alama2)**

**(q)** Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili **(alama2)**

**(r)** Akifisha kifungu kifuatacho: **(alama4)**

Mzee alimwambia mwanawe njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue mtoto aliuliza nani babu?

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K12

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno **(alama2)**

**(b)** Onyesha matumizi ya kiambishi 'ku' katika sentensi ifuatayo**:** **(alama2)**

Amani atakutengenezea mpini wa jembe kisha akaaelekee kule kwao.

**(c)** Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Irabu ya mbele wastani

**(ii)** Kipasuo ghuna cha kaakaa laini

**(d)** Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya YA – Ya kutunga sentensi. **(alama2)**

**(e)** Tunga sentensi moja katika wakati ujao hali timilifu **(alama2)**

**(f)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

KN(N) + KT(T+E) +U + KN(N) + KT(T+E)

**(g)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi changamano **(alama2)**

**(h)** Tunga sentensi kutofautisha maana ya: **koga** na **konga** **(alama2)**

**(i)** Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii **(alama2)**

**(j)** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano **(alama3)**

**(i)** Nywa(tendesha)

**(ii)** La(tendeana)

**(iii)** Vaa(tendwa)

**(k)** Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana tatu tofauti**.** **(alama3)**

Julius Kiptoo mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa

**(l)** Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari. Naam ameleta machache. **(alama2)**

**(m)** Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu **(alama1)**

**(n)** **(i)** Eleza maana ya shadda **(alama1)**

**(ii)** Onyesha panapotokea shadda katika neno mteremko **(alama1)**

**(o)** Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**

Sahibu yake alishikwa na kisunzi.

**(p)** Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari **(alama3)**

Ubaguzi wa kijinsia umekasifiwa na viongozi wenye misimamo thabiti mno.

**(q)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa: **(alama2)**

"Shughuli yetu itamalizika kesho," mama alimwambia Juma.

**(r)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Watahiniwa hao walisoma maswali yote kwa makini.

**(s)** Ainisha sentensi kwa kuzingatia jukumu/dhamira **(alama1)**

Funga majani matano matano kwa kila fungu

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K13

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a) (i)Eleza maana ya sauti mwambatano** **(alama1)**

**(ii)**Taja sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye masine **(alama1)**

**(b)** Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kielezi **(alama1)**

Komu ameshona nguo <u>nzuri</u> na kuiuza sokoni.

**(c)** Tunga sentensi moja moja kubainisha **(alama2)**

**(i)** Kihusishi cha wakati

**(ii)** Kivumishi cha pekee chenye maana ya bila kubagua

**(d)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi: **(alama2)**

Askari wasipopiga doria wala hushirikana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama.

**(e)** Bainisha mofimu katika neno: **(alama3)**

Atamnywea

**(f)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo: **(alama2)**

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi

**(g)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake.

**(h)** Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi matatu ya kiambishi 'li' **(alama3)**

**(i)** **(i)** Eleza maana ya sentensi ya masharti **(alama1)**

**(ii)** Tunga sentensi ya masharti **(alama2)**

**(j)** Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha **(alama2)**

**(i)** Umilikaji

**(ii)** Nafasi katika orodha au nafasi katika kundi

**(k)** Tunga sentensi yenye kikundi chenye muundo ufuatao: **(alama2)**

Kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino

**(l)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumzi mawili tofauti ya kistari kirefu **(alama2)**

**(m)** Unganisha sentensi zifuatazo bila kurudia kitenzi **(alama2)**

Osore amempigia Ngungui simu. Ngungui amempigia Osore simu

**(n)** Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha vitenzi vilivyomo kuwa nomino: **(alama2)**
Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana.

**(o)** Andika maana tatu ya neno: kanda **(alama3)**

**(p)** Andika visawe viwili vya nahau: enda kombo. **(alama2)**

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K14

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** **(i)** Ni nini maana ya silabi **(alama1)**

**(ii)** Tunga neno lenye muundo huu wa silabi **(alama1)**

Irabu + konsonanti + konsonanti + irabu

**(b)** Ainisha vitenzi katika sentensi **(alama3)**

Ndege yu taabani, hata hivyo anajaribu kujinasua.

**(c)** Geuza sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo: **(alama2)**

Wachezaji hawakucheza mpira kwa sababu ya mvua.

(Anza kwa: Mpira…)

**(d)** Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu **(alama2)**

Dobi huwapigia watu nguo pasi.

**(e)** Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**

<u>Ubora</u> wa kazi zao <u>ulifichika baada ya kuanzishwa</u> kwa mradi ule.

**(f)** **(i)** Eleza maana ya kirai **(alama1)**

**(ii)**Ainisha virai vilivyopigiwa mstari **(alama2)**

Zana hizi zimeundwa <u>na mafundi wenye</u> <u>ustadi mkubwa</u>.

**(g)** Kinga ni hali ya kuzuia madhara fulani. Andika maana nyingine mbili za 'kinga' **(alama2)**

**(h)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi **(alama2)**

Lililimwa vizuri sana

**(i)** Bainisha maana ya mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Wakimbizi walisema kuwa walitamani kurudi kwao mwaka huo.

**(j)** Andika sifa mbili za sauti ifuatayo /dh/ **(alama2)**

**(k)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja **(alama2)**

Hao wenyewe hawakuzigatia mafunzo ya lishe bora.

**(l)** Tunga sentensi moja kubainisha tofauti ya kimaana kati ya gharama na karama

**(alama2)**

**(m)** Kanusha sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Wanafunzi waliingia darasani, wakatoa vitabu wakaanza kusoma.

**(n)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya nukta pacha **(alama2)**

**(o)** Tumia nomino ya jamii kuwakilisha maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**

<u>Nzege wengi sana</u> walivamia na kuharibu mimea.

**(p)** Onyesha visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari **(alama1)**

Washiriki wote walituzwa <u>medali</u> baada ya <u>mchuano</u> huo.

**(q)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Furaha

**(ii)** Nyasi

**(r)** Unganisha sentensi hizi uitumia Kiunganishi cha kinyume **(alama2)**

Wananchi walikabiliwa na hatari

Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi

**(s)** Andika upya sentensi ukianza kwa yambwa tendwa **(alama2)**

Wafugaji waliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K15

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika sauti zenye sifa zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Nazali ya kaakaa laini

**(ii)** Kikwamizo ghuna cha mdomo na meno

**(iii)** Irabu ya nyuma, wastani

**(iv)** Kiyeyusho cha kaakaa gumu

**(b)** Bainisha silabi katika neno wanyweshavyo **(alama1)**

**(c)** Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi. **(alama2)**
Wafanyakazi wote watafanyiwa tathmini ili kupata suluhu ya matatizo hayo.

**(d)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja **(alama2)**
Mkihifadhi nafaka hizo vizuri maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha.

**(e)** Andika neno lenye mofimu zifuatazo: **(alama2)**
Nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendesha, kauli tenda

**(f)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: kama **(alama2)**

**(i)** Kiunganishi

**(ii)** Kihusishi

**(g)** Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi **(alama2)**

**(h)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. **(alama1)**

Nyumba hizo zilijengwa mbali na mji ule.

**(i)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

Nomino ya jamii, kirai kihusishi, kitenzi kishirikishi, kielezi cha mahali

**(j)** Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo **(alama1)**

Chakula kinachozalishwa kwa njia za kiasili kina viinilishe vingi.

(Anza kwa: Viinilishe vingi…)

**(k)** Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mistari **(alama1)**

<u>Mtalii</u> atazuru <u>mbuga</u>

**(l)** Akifisha sentensi ifuatayo. **(alama3)**
basi mwanangu akasema daudi hivyo tunavyoweza kufikiria vision 2030 wewe waonaje

**(m)** Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati **(alama1)**

Beti alijishindia tuzo.
Beti alishiriki katika utunzaji wa mazingira.

**(n)** Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha **(alama2)**

**(i)** Sababu

**(ii)** Pamoja na

**(o)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. **(alama3)**

Mvua ilinyesha tulipokuwa tukilima.

**(p)** Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa **(alama2)**

Malik alipuliza siwa akiwa kwa Shaka.

**(q)** Onyesha matumizi ya 'ka' katika sentensi ifuatayo: **(alama1)**

Mumbi alitia embe kapuni likaiva.

**(r)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. **(alama3)**

Mmomonyoko wa udongo ulipozuiliwa mashamba yalinawiri.

**(s)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya vito na fito **(alama2)**

**(t)** Methali: mzigo wa mwenziwo ni kanda la usufi, huambiwa mtu anayezidharau shida za wengine. Mtu asiyetambua kuwa kuna wengine wanaoweza kulimudu jambo kuliko yeye huambiwa methali gani? **(alama1)**

**(u)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mwenyewe alikipenda kwa dhati.

**(v)** Tunatumia kihisishi makiwa tunapotaka kumtuliza aliyefiwa na **................**tunapotaka mtu atupishe. **(alama1)**

**(w)** Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba tendo lilifanikiwa kwa sababu ya kufanikiwa kwa tendo jingine **(alama1)**

**(x)** Andika nahau inayojumuisha ujumbe ufuatao: **(alama1)**

Kumzuia mtu kupata kitu japo huna haja nacho.

**(y)** Shambi ni kwa udongo, **......................** kwa chumvi, na **.......................**kwa mtama **(alama1)**

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K16

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tumia nomino yoyote katika ngeli ya I –I kutunga sentensi **(alama1)**

**(b)** **(i)** Ni nini maana ya silabi **(alama1)**

**(ii)** Tunga neno lenye muundo huu wa silabi **(alama1)**
Irabu + konsonanti + konsonanti + irabu

**(c)** Tunga sentensi hii upya kwa kufuata maagizo: **(alama2)**
Wasichana wanaingia darasani kwa haraka.
(Andika kinyume)

**(d)** Tambua kiambishi awali na tamati katika neno: **(alama2)**

alalaye

**(e)** Ainisha vivumishi katika sentensi hii **(alama4)**

Mzee mwenyewe ni mkongwe na amepewa zawadi kwa kuwa shamba lake lilitoa mazao mengi.

**(f)** Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama.

(Yakinisha sentensi hii) **(alama2)**

**(g)** "Shughuli yetu itakamilika kesho, mama alimwambia mwanawe Juma."

(Andika katika usemi wa taarifa) **(alama2)**

**(h)** Changanua sentensi kwa kielelezo cha matawi **(alama3)**

Mpira ulichezwa tulipokuwa tukipika.

**(i)** Dhihirisha matumizi matatu tofauti ya kimaana yanayotokea katika kitenzi 'ona' kikinyambuliwa katika kirai 'ona ndoto' **(alama3)**

**(j)** Eleza matumizi ya hali za, ka na hu katika sentensi zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Balozi huja hapa kila mara

**(ii)** Mpishi alipika, akapakwa na akagawa chakula.

**(k)** Eleza maana mbili za sentensi: **(alaama2)**

Tuliitwa na baba

**(l)** Akifisha: **(alama4)**

Shangazi alimwambia mwanawe njoo nikupelekee kwenu jioni mtoto aliuliza kwetu wapi

**(m)** Eleza matumizi mawili ya kiambishi 'ji' **(alama2)**

**(n)** Tunga sentensi hii upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari **(alama3)**

Ukuta umemwumiza mvulana alipokuwa akiuparaga.

**(o)** Tukia kitenzi –fa- katika sentensi kuonyesha mazoea **(alama2)**

**(p)** Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Baba alifika mapema kuliko wote halafu akaondoka.

**(q)** Tumia kitenzi "tafakari" kama nomino katika sentensi **(alama1)**

**(r)** Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mstari **(alama1)**

Mwanamuziki atautembelea mji.

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K17

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika tofauti moja kati ya sauti zifuatazo **(alama2)**
- **(i)** /ng'/ na /gh/
- **(ii)** /v/ na /f/
- **(iii)** /r/ na /l/
- **(iv)** /m/ na /n/
- **(v)** /s/ na /z/

**(b)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo: **(alama2)**
- **(i)** Konsonanti, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu
- **(ii)** Konsonanti, konsonanti, irabu konsonanti, irabu

**(c)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi 'o' **(alama2)**

**(d)** Andika sentensi zifuatazo upya kulinga na maagizo: **(alama2)**
- **(i)** Mhalifu alisemehewa kwa sababu alinyenyekea.
  (Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino)
- **(ii)** Waigizaji wengine wameingia jukwani.
  (Tumia kivumishi cha idadi chenye kuonyesha nafasi katika orodha

**(e)** Tunga sentensi ukitumia kirai kihusishi kama kielezi **(alama2)**

**(f)** Unganisha sentensi zifuatazo kwa viunganishi mwafaka **(alama2)**
- **(i)** Kheri aliweza kutujengea hospitali. Atajenga zahanati pia.
- **(ii)** Zumari anasoma uanasheria. Vilevile Maki anasomea uanasheria.

**(g)** Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya A – WA **(alama2)**

**(h)** Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika **(alama2)**

**(i)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja **(alama2)**
Maseremala walilainisha mbao hizo wakatutengenezea meza.

**(j)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama2)**
- **(i)** Kaumu amewafanya mifugo wangu wanywe maji.
  (Anza kwa: Mifugo, usitumie; amewafanya")
- **(ii)** Wanakijiji wanaishi karibu na msitu. Wananchi hawavamii wanyama.
  (Unganisha kuunda sentensi ambatano)

**(k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama1)**
Ngoma hizo zao ziliibwa na wezi wale.

**(l)** Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha: **(alama2)**
- **(i)** Sehemu ya kitu kizima.
- **(ii)** Namana tendo lilifanyika

**(m)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama2)**
"Kusoma kwa mapana kutapalilia ubunifu wa wanafunzi hawa wenu," mtaalamu akatuambia.

**(n)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Viwanda vikianzishwa mashambani idadi ya wanaohamia mjini itapunguzwa.

**(o)** Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo **(alama2)**
- **(i)** KN (N+ RH) + KT (TS + T)
- **(ii)** KN (V+N) + KT(t+V)

**(p)** Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Mhunzi alimfulia mjukuu wake pete ya shaba.

**(q)** Bainisha maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Bedua alimrushia tufe.

**(r)** Alama za mtajo hutumiwa kufungia maneno halisi ya msemaji. Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mengine mawili ya alama za mtajo **(alama2)**

**(s)** Andika sentensi ifuatayo kwa kutumia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**
Mwanafunzi <u>mkakamavu</u> <u>huzingatia</u> masomo yake.

**(t)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya rithi na ridhi **(alama2)**

**(u)** Tunatumia sile tunapotaka mtu atupishe……………………… tunapoomba kitu kinusurike, na kefule …………………………… Na jambo. **(alama1)**

**(v)** Andika visawe vya maneno yafuatayo: **(alama1)**
- **(i)** Doa
- **(ii)** Omba

**(w)** Andika sentensi ifuatayo upya kulingana na maagizo **(alama1)**
Maeneo haya yana uyoga.
(Anza kwa: Uyoga…)

# DARUBINI SERIES ~2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K18

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika sauti zenye sifa zifuatazo: **(alama2)**

**(i)** Kipasuo ghuna cha midomoni

**(ii)** Irabu ya kati, chini

**(iii)** Kikwamizo ghuna cha kaakaa gumu

**(iv)** Nazali ya ufizi

**(b)** Bainisha silabi zilizowekwa shadda katika maneno yafuatayo **(alama1)**

**(i)** Miambakofi

**(ii)** Yatazoleka

**(c)** Andika neno lenye muundo ufuatao **(alama2)**

**(i)** Kiambishi ngeli, wakati uliopita, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda (kiishio)

**(ii)** Kiambishi cha wingi, mzizi

**(d)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama4)**

**(i)** **Uaminifu** wa watu humfanya aheshimiwe.

(Badilisha nomino iliyopigiwa mstari kuwa kivumishi)

**(ii)** Shama, Tegea na Koru ndio walioibuka washindi.

(Tumia kivumishi nafsi badala ya maneno yaliyopigwa mstari)

**(i)** Mchuuzi alinunua mboga zilizofungwa pamoja.

(Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari)

**(ii)** Selume ni mtiifu. Maria ni mtiifu pia.

(Unganisha kuwa sentensi moja yenye kihusishi cha kulinganisha)

**(e)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama1)**

**(i)** Ugwe

**(ii)** Limau

**(f)** Unganisha sentensi zifuatazo kuunda sentensi ya masharti **(alama2)**

Moto ulidhibitiwa. Kulikuwa na vifaa vya kutosha.

**(g)** Andika sentensi ifuatayo kwa wingi: **(alama2)**

Nahodha alilikwepa jabali hilo, chombo kikafika ufuoni salama.

**(h)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

Nomino, kishazi tegemezi, kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi

**(i)** Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya mazoea **(alama1)**

Barabara nyingi zimesakafiwa.

**(j)** Unganisha sentensi zifuatazo kwa kuanza kwa neno: Wanafunzi… **(alama2)**

Wageni wamefika. Wanafunzi wamefurahi.

**(k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama1)**

Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hilo zinavutia.

**(l)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama2)**

**(i)** Muutu aliwalea watoto wa Maki.

(Anza kwa: Watoto wa Maki…)

**(ii)** Maji yalijaa.

Maji yalimwagika.

(Unganisha kuwa sentensi changamano)

**(m)** Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari **(alama1)**

Sewe alitueleza jambo hilo <u>kinagaubaga</u>.

**(n)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Viongozi wengi walikuwa waadilifu mno kabala ya uchaguzi mkuu.

**(o)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari **(alama2)**

**(i)** Mkufu wa Umu unapendeza mno.

**(ii)** Hili lake lilikuwa limeiva lakini hatukujua.

**(p)** Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Medi anasema atawarithisha nyuma yake.

**(q)** Akifisha sentensi ifuatayo **(alama2)**

Jihadhari akasema kulei uamuzi wako unaweza kukuathiri vibaya

**(r)** Kanusha sentensi ifuatayo **(alama1)**

Mkulima anahitaji magunia haya.

**(s)** **(i)** Karimu kwa mchoyo …………………………… ni kwa kukashifu na…………………. ni kwa tele **(alama2)**

**(ii)** Maarufu ni kwa mashuhuru, ukoo ni kwa ……………… ilhali faida ni kwa …………………… **(alama2)**

**(t)** Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: kata **(alama2)**

Watu wa Kata ya Madogo wamezoea kukata miti hivyo.

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K19

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo **(alama2)**

**(i)** Irabu, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti irabu.

**(ii)** Konsonanti, konsonanti, irabu, irabu.

**(b)** Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Asemavyo

**(ii)** Mwangwi

**(c)** Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Shule nzima ilifurahia ukarimu wa shirika la Tugawane.

**(d)** Andika sentensi ifuatayo katika wingi. **(alama1)**

Seremala aliulainisha ubao huo ili kutengeneza kasha amuuzie mlinzi huyo.

**(e)** Tunga sentensi ukitumia vivumishi vinavyotoa maana zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Nafasi katika orodha

**(ii)** Kutobagua

**(f)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama2)**

Mtu huyo alifuata njia iliyomwelekeza mjini.

**(g)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama2)**

**(i)** Mhandisi alikarabati mtambo. Mtambo ulikuwa kiwandani.

(Unganisha kuwa sentensi moja bila kutumia kiunganishi)

**(ii)** Kembo alishona fulana hiyo vizuri sana.

(Tumia kielezi cha kiasi badala ya vile vilivyopigiwa mstari)

**(h)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi **(alama2)**

Mkurugenzi alisema kwamba wangetoa nyongeza ya mshahara mwaka ambao ungefuata.

**(i)** Geuza sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu **(alama1)**

Ni wazi kuwa gharama ya maisha itapanda bei ya mafuta ikipanda.

**(j)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama1)**

Badi huwa hapitii hapa, huenda usimpate.

**(k)** Zuri ni kwa baya, aminifu ni kwa ………………… na vivu ni kwa…………… **(alama2)**

**(l)** Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Sukari

**(ii)** Teo

**(m)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari **(alama2)**

Mvua imepusa na watu wameanza kuondoka.

**(n)** Vyakula viliandaliwa. Vyakula vilikuwa na viinilishe muhimu.

(Unganishi kuunda sentensi changamano) **(alama2)**

**(o)** Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Zumari alimtunzia Keto watoto hao upendo.

**(p)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi 'ku' **(alama2)**

**(q)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Usalama ukiimarishwa watalii wengi watakuwa wanazuru humu.

**(r)** Unaporidhika na jambo unasema hewala, unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi unasema ………………………. na unapotaka usikivu unasema……………………………………… **(alama2)**

Unaposhangilia timu yako unasema <u>…………….</u> na upotaka utulivu unasema **kimya**

**(s)** Jepesi ni kwa rahisi, ukuta ni kwa ……………………, na njia kwa ………….. **(alama2)**

**(t)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya dua na tua **(alama1)**

**(u)** Mzee Pumu ni mraibu wa vileo. Baada ya muda watoto wake wawili wanakuwa watumizi sugu wa vileo. Andika methali inayoweza kutumiwa kueleza hali hii **(alama1)**

**(v)** Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha utenzi. **(alama2)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K20

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo: **(alama2)**

**(i)** Kipasuo ghuna cha midomoni, irabu ya chini kati, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya juu mbele

**(ii)** Nazali ya ufizi, kipasuo, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu nyuma, irabu ya nyuma wastani

**(b)** Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo: **(alama1)**

**(i)** Waliotusifia

**(ii)** Sherehekea

**(c)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja. **(alama1)**
Nyua walizojenga hapa zimesaidia kukabiliana na wahalifu hao.

**(d)** Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo: **(alama1)**
Mbuzi huyu wake ana ngozi laini

**(e)** Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na kivumishi kimilikishi **(alama1)**

**(f)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama8)**

**(i)** Maafisa hao walipewa uhamisho.
Maafisa wengine hawakupewa uhamisho.
(Unganisha kuunda sentensi ambatano)

**(ii)** Hadithi hiyo <u>ilitungwa</u> vizuri <u>ikawavutia</u> wengi.
(Badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa nomino)

**(iii)** Tunda halitaoshwa vyema. Tunda halitalika.

(Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia kutumia 'po'

**(iv)** Kongewa alitopa ahadi. Wengi waliamini ahadi hiyo.

(Unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa: Ahadi…)

**(g)** Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine **(alama2)**

**(h)** Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi **(alama2)**

**(i)** Ainisha maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo **(alama3)**
<u>Mwenyewe hakuwa amekupa</u> ruhusa kuitumia.

**(j)** Akifisha sentensi ifuatayo: **(alama2)**

mwanangu akasema Neema huku amemkazia macho huoni unamtia mwenzako wasiwasi

**(k)** Andika maneno yenye mofimu zifuatazo **(alama3)**

**(i)** Umoja (ngeli ya U-I), mzizi, kiishio

**(ii)** Nafsi, mzizi kauli, kirejeshi

**(iii)** Kikanushi, kiambishi ngeli (KI – VI umoja), mzizi kauli ya kutendeka kiishio

**(l)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

KN (N+RH) + KT (T+E)

**(m)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha **(alama1)**

Ngoma hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini

**(n)** Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya mazoea. **(alama2)**

Bili atawashauri vijana kuhusu umuhimu wa michezo.

**(o)** Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**

Alimfanya Tindi **anywe** pombe ikamfanya **alewe**.

**(p)** Tunga sentensi ukitumia mzizi, -ingine kumaanisha "baadhi ya" **(alama2)**

**(q)** Hewala ni kwa kukubaliana na jambo, __________ ni kwa kutaka kitu kinusurike, na _________________ ni kwa aliyefanya vyema katika jambo **(alama1)**

**(r)** Zito ni kwa jepesi ,……………. ni kwa choyo, na ………………….ni kwa kali **(alama1)**

**(s)** Andika visawe vya kauli zilizopigwa mstari **(alama2)**

Musei **alikumbwa** na matatizo mengi lakini **hakukata tamaa.**

**(t)** Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: zima. **(alama2)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K21

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Tofautisha sauti zifuatazo: **(alama2)**

**(i)** /l/ na /r/

**(ii)** /m/ na /b/

**(b)** Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi ifuatayo: **(alama1)**

Wasaidieni wale, walinisaidia wakati wa shida.

**(c)** Andika neno moja lenye silabi za muundo ufuatao: **(alama1)**

Konsonanti + konsonanti + irabu + konsonanti + konsonanti + irabu

**(d)** Tunga sentensi kubainisha kiunganishi kitegemezi **(alama2)**

**(e)** Tumia neno 'vile' katika sentensi kama: **(alama2)**

**(i)** Kivumishi

**(ii)** Kielezi

**(f)** Kutokana na mzizi '-erevu' unda **(alama2)**

**(i)** Nomino

**(ii)** Kivumishi

**(g)** Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Chanda

**(ii)** Teo

**(h)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Wale wengine wataelekea ughaibuni kwa ndege

**(i)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja. **(alama1)**

Nguo walizouza madukani mwao ziliwavutia watalii.

**(j)** Geuza sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama1)**

Makuli hawajakuarifu kwamba mizigo hiyo haikuwa yetu?

**(k)** Akifisha sentensi ifuatayo **(alama2)**

lo kandio hamadi ndiye mwandishi wa kisiwa chenye tunu

**(l)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi **(alama2)**

Mama alimwita Juma na kutaka kujua namna alivyofaulu kuuzima moto huo.

**(m)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo: **(alama2)**

Seremala alilainisha mbao. Seremala alikuwa kiwandani

(Unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa mbao bila kubadilisha maana.)

**(n)** Andika kinyume cha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari **(alama1)**

Punde tu <u>alipouliza</u> swali hilo Koru <u>aliingia</u> darasani.

**(o)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea **(alama1)**

Jani ambalo lilipukutika lilipeperushwa na upepo.

**(p)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari **(alama2)**

Wakulima hawa walipanda zao hili daima.

**(q)** Andika sentensi ifuatayo upya ukianza kwa yambwa tendewa **(alama2)**

Andai alimnywesha babu uji kwa kikombe.

**(r)** Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno **somo** **(alama2)**

**(s)** Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya 'kwa' **(alama2)**

**(i)** Sehemu ya kitu

**(ii)** Namna

**(t)** Tunga sentensi moja kubainisha kishazi huru na kishazi kitegemezi **(alama2)**

Wageni waliofika leo wametufurahisha

**(u)** Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Fundi alimkatia Makaa utepe huo.

**(v)** Zimwi zilizidi kukimbia. Shujaa aliongeza mwendo kulifikia.

(Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia neno kadiri) **(alama2)**

**(w)** Tunga sentensi kuonyesha majukumu yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Sentensi agizi

**(ii)** Sentensi hisishi

# DARUBINI SERIES ~ 2025

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K22

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2025 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika irabu zenye sifa zifuatazo: **(alama1)**

**(i)** mbele, juu, tandazwa

**(ii)** nyuma, wastsni, viringwa

**(b)** Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo: **(alama1)**

**(i)** Bingiria

**(ii)** Walimwengu

**(c)** Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Mfariji

**(ii)** Anavyojenga

**(d)** Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mkulima yupo shambani anapalilia mimea.

**(e)** Andika sentensi ifuatayo kwa umoja **(alama1)**

Waashi walijenga majumba ya kifahari ya kupendeza.

**(f)** Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo **(alama1)**
Wahandisi walikarabati barabara zote baada ya mafuriko.
(Anza kwa: Barabara….)

**(g)** Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: **(alama1)**

**(h)** Alama ya mshazari hutumiwa kutenga nambari. Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mengine ya alama ya mshazari **(alama1)**

**(i)** Kanusha sentensi ifuatayo: **(alama1)**
Wanariadha wameenda uwanjani kufanya mazoezi.

**(j)** Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo.

**(i)** Watalii walifika katika mbuga ya Tsavo walikowanaona wanyamapori.

(Tumia 'amba') **(alama1)**

**(ii)** Mkurugenzi aliwashauri wafanyakazi wajibidiishe kazini.

(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino) **(alama2)**

**(k)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Vipepeo wale weupe wanaashiria mvua ya masika inayotarajiwa mwakani.

**(l)** Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo: **(alama3)**

Wanakijiji waliwajengea wakongwe nyumba kwa mawe.

**(m)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea **(alama2)**

Huduma za afya zilipoboreshwa, viwango vya maambukizi vilipungua.

**(n)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama2)**

"Watunza mazingira watanadhifisha soko letu kesho." Chifu aliwaambia wafanyabiashara.

**(o)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi '-ka' **(alama2)**

**(p)** Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Bendera

**(ii)** ujana

**(q)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo **(alama2)**

Ngoma hizo zimetenenezwa kwa ngozi laini.

**(r)** Tunga sentensi ukitumia kihisishi kinachoibua hisia za kinyume cha matarajio **(alama1)**

**(s)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

KN (N+S) +KT (T) + KN (N+V)

**(t)** Bainisha maana mbili zinazojitokeza katika ifuatayo: **(alama2)**

Jena angalifuata ushauri wa mwelekezi wake angalifaulu.

**(u)** Baraste ni kwa barabara, hekima ni kwa ……………… na sihi ni kwa**………..(alama2)**

**(v)** Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno hema **(alama2)**

**(w)** Rafiki yako ana mazoea ya kutoa visababu ili asifanye kazi fulani. Andika methali unayoweza kutumia kumwonya dhidi ya tabia hiyo **(alama1)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K23

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Sauti /b/ katika neno bora ni kipasuo cha midomoni. Andika sifa mbili za sauti iliyoandikwa kwa herfi nzito: ng'o**a** **(alama1)**

**(b)** Bainisha silabi katika neno lifuatalo: **(alama2)**
tunza

**(c)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: **(alama2)**
Mlizoleta

**(d)** Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha neno lililopigwa mstari kuwa nomino **(alama2)**

Barabara nzuri ziliufanya mji <u>uvutie.</u>

**(e)** Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia "ki" ya masharti **(alama2)**
Juma angekamilisha mradi huomapema angekihakishia kijiji chake usalama wa haraka

**(f)** Akifisha sentensi ifuatayo: ajabu mwezi wa januari una mvua **(alama2)**

**(g)** Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo **(alama1)**
Mwenye bidii atatuzwa hadharani

**(h)** Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita timilifu. **(alama2)**
Vyumba katika bweni lile vinapakwa rangi.

**(i)** Bainisha kirai kivumishi na kirai elezi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Mwanafunzi yule mwadilifu alifika mapema mno.

**(j)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama1)**
Barabara hizi zilikarabatiwa mwaka jana.

**(k)** Bainisha matumizi mawili ya 'po' katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Maria hushangiliwa sana anapoimba.

**(l)** Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

**(i)** Wanakijiji walifika kwa wakati kuzoa taka.
Gari la kubeba taka lilichelewa.
(Unganisha kwa kutumia ingawa) **(alama2)**

**(ii)** Katana alichukua stakabadhi zote zilizohitajika akazitia kwenye faili.
(Kanusha) **(alama2)**

**(iii)** Rita alimrai Waridi amfunze kucheza kandanda
(Tumia kisawe cha neno lililopigiwa mstari) **(alama1)**

**(m)** Tunga sentensi yenye vishazi viwili huru **(alama2)**

**(n)** Kiambishi wa katika kitenzi wanasaidia kinaonyesha mtenda. Tunga sentensi yenye kiambishi 'ku' cha yambwa **(alama2)**

**(o)** Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

**(i)** Helikopta iliyobeba wanajeshi hao ilipaa angani saa tano asubuhi.

(Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari) **(alama2)**

**(ii)** Vyumba vya kurekodia nyimbo vina mwangwi.

(Andika katika umoja) **(alama2)**

**(iii)** Kanini aliwapikia pilau watoto wa Aisha.

(Anza kwa: watoto….) **(alama2)**

**(p)** **Angua** ni tendo la kutoa matunda mtini. Angua pia ni? **(alama2)**

**(q)** Tunga sentensi ukitumia kwa kuonyesha 'nia' **(alama2)**

**(r)** Nomino 'bidii' imo katika ngeli gani? **(alama1)**

**(s)** Robot ani kwa pamba, tita ni kwa …………. na ………….. ni kwa blanketi **(alama2)**

**(t)** Haba na haba hujaza kibaba ni methali inayotumiwa kuonyesha umuhimu wa kuthamini na kuvihifadhi vitu vichache tulivyo navyo kwa kuwa vikiwekwa pamoja huwa vingi, vikakidhi haja.

Andika methali unayoweza kutumia kumhimiza mwenzako kutenda mambo mazuri. **(alama1)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## K24

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika neno lenye kitamkwa cha ufizi **(alama1)**

**(b)** Onyesha silabi inayotamkwa kwa mkazo katika neno: Uliopandwa. **(alama1)**

**(c)** Eleza majukumu ya viambishi katika neno: vikimvutia **(alama2)**

**(d)** Andika upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo. **(alama8)**

**(i)** Mabaharia walifika bandarini.

Walikuwa wamesafiri kwa wiki moja.
(Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia kihusishi cha wakati)

**(ii)** Kurugenzi alimpandisha cheo afisa husika ambaye alivumbua huduma hiyo.

(Andika upya kwa kugeuza kitenzi kilichopigiwa mstari kuwa nomino bila kubadilisha maana)

**(iii)** Wanakijiji wataweka mikakati ifaayo.

Watajitosheleza kwa chakula.

(Unganisha kuunda sentensi changamano)

**(iv)** Barabara hiyo itapitia Shazi.

(Kanusha kwa kuanza kwa neno: Shazi…)

**(e)** Tunga sentensi zenye vihisishi vinavyoibua hisia zifuatazo:

**(i)** Kinyume cha matarajio
**(ii)** Kutaka kitu kinusurike

**(f)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja **(alama2)**

Makasha hayo yaliyotengenezwa viwandani na mafundi hao yaliwanufaisha.

**(g)** Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama1)**

Nguo zenyewe zilihifadhiwa kwenye vikapu.

**(h)** Tunga sentensi katika wakati uliopo kuonyesha kwamba kitendo kimekuwa kikiendelea kwa muda **(alama1)**

**(i)** Andika sentensi ifuatayo kwa kuanza kwa yambwa tendwa **(alama2)**

Vijana walisafisha soko la kijiji chao.

**(j)** Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi **(alama2)**

Chifu aliwakumbusha walezi kwamba walihitaji kuwapeleka watoto kwa chanjo dhidi ya polio Ijumaa ambayo ingefuata.

**(k)** Bainisha maana tatu katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Mandila aliwatangazia chao.

**(l)** Kistari kifupi hutumiwa kutenga silabi. Vilevile, huweza kutumiwa kudokeza hoja. Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mengine mawili ya kistari kifupi **(alama2)**

**(m)** Tunga sentensi kuonyesha muundo ufuatao: **(alama2)**

KN(N+V) KT(T+KH) + U+ KN (0) +KT(T+E)

**(n)** Bainisha matumizi ya kwa katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

**(o)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** mafuta

**(ii)** kwato

**(p)** Tumia nahau badala ya maneno yaliyopigiwa mstari **(alama1)**

Tuta **<u>aliwaomba msamaha</u>** wazazi wake.

Tuta **aliwaangukia miguuni** wazazi wake.

**(q)** Kusimulia ni kwa kutamba ………………….. ni kwa adabu na …………………….. ni kwa imara **(alama2)**

**(r)** Methahli, jifya moja haliinjiki chungu huambiwa kwa mtu ambaye haoni umuhimu wa kushirikiana na wengine. Ni methali ipi ambayo huambiwa mtu ambaye anadharau vitu duni ambavyo vinaweza kumfaa wakati wa shida. **(alama1)**

**(s)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya ____________________________ na ______________ **(alama2)**

**(t)** Jirani yako ameshukiwa kufanya kosa na kutiwa ndani. Atalipa ……………………… ili kuachiliwa kwa muda kesi ikisikilizwa **(alama1)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 001

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Dondoa sauti mwambatano katika maneno yafuatayo na utambue mahali sauti hiyo hutamkwa **(alama2)**

**(i)** Ngwena

**(ii)** Pwaguzi

**(b)** Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa **(alama2)**

**(i)** Oa

**(ii)** Cha

**(c)** Andika katika wingi **(alama1)**

Nywa

**(d)** Onyesha muundo wa silabi ya katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Ngamia

**(ii)** Ng'ombe

**(e)** Ainisha vipashio vya kisarufi katika fungutenzi lililopigiwa mstari **(alama3)**

<u>Sikumkaribisha</u> huyo mwalimu.

**(f)** Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

**(i)** Wezi hawa walivuka mito hii.
(Tumia vivumishi visisitizi badala ya viashiria.) **(alama2)**

**(ii)** Tulitoa kodi kubwa kwenye serikali.
(Anza: Kodi…) **(alama2)**

**(iii)** Wanafunzi walimwahidi mwalimu wangejitahidi pale shuleni ili wapite mtihani wao.
(Geuza kuwa katika usemi halisi) **(alama2)**

**(g)** Fafanua matumizi ya **'kwa'** na **'ki'** katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Wakubwa kwa wadogo walikuja kwa gari moshi kuona kitoto kilichozaliwa kimiujiza.

**(h)** Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia vigezo viwili vya kuainisha sentensi **(alama2)**

Anastacia amemlaumu Brenda ilhali kosa lilikuwa la Gesare.

**(i)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea **(alama2)**

Malipo ambayo anapewa ni yale ambayo yanamridhisha.

**(j)** Changanua sentensi hii kwa matumzi ya jedwali **(alama4)**

Wanafunzi wengi wameenda nyumbani lakini yeye amebaki shuleni.

**(k)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**

**(i)** Redio

**(ii)** Mawaidha

**(l)** Ainisha vishazi vitegemezi katika sentensi zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Iwapo atafika nyumbani leo, atampata baba.

**(ii)** Mpira ambao ni mpya umepotea.

**(m)** Andika kinyume cha sentensi hii **(alama1)**

Kaubane mlango kisha umtwike mchukuzi mzigo huo.

**(n)** Onyesha aina za yambwa katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Amemnunulia mtoto kifunguamimba gari kubwa mno.

**(o)** Yakinisha: Fasihi simulizi haina athari ya kudumu kwa fasihi andishi. **(alama1)**

**(p)** Tunga sentensi ukitumia vihusishi vya 'a' unganifu vyenye dhana zifuatazo **(alama3)**

**(i)** Uhusiano wa wakati

**(ii)** Nafsi katika orodha

**(iii)** Umilikaji

**(q)** Eleza maana mbili zinazoweza kujitokeza katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Jane angalifuata ushauri wa mwelekezi wake angalifaulu.

**(r)** Taja kazi ya kihisishi katika sentensi ifuatayo **(alama1)**

Kefule! Tangu lini mzazi akamlaaani mwanawe.

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 002

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** **(i)** Toa mfano wa konsonanti ambayo ni kipasuo - kwamizo **(alama1)**
**(ii)** Fafanua dhana ya sauti mwambatano **(alama2)**

**(b)** Ainisha vipashio vya kisarufi katika neno hili **(alama3)**
Sikumkaribisha

**(c)** Yakinisha sentensi ifuatayo **(alama2)**
Hakuwasaidia wala hakuwakaribisha kwake jana.

**(d)** Tambua matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Kiti ki jikoni baada ya kuangushwa na kijitu kile.

**(e)** Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo **(alama2)**
**(i)** Walimwengu
**(ii)** Katakata (kugawa vipande)

**(f)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**
**(i)** Maradhi
**(ii)** Chai

**(g)** Tambua aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo **(alama3)**
Ilitumiwa kumlimia nyanya yake shamba lile. Yake ilioshwa kwa sabuni.

**(h)** Ainisha sentensi ifuatayo kidhamira na kimuundo **(alama2)**
Soka ni mchezo maarufu mno ulimwenguni.

**(i)** Onyesha muundo wa silabi katika neno lifuatalo **(alama1)**
Mchwa

**(j)** Changanua sentensi ifuatayo kwa matumizi ya matawi **(alama3)**
Vile vingali vikitengenezwa

**(k)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vivumishi vifuatavyo **(alama3)**
**(i)** Kivumishi cha idadi kamili
**(ii)** Kivumishi kimilishi (ngeli ya KU)
**(iii)** Kivumishi cha pekee bila kubagua

**(l)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama3)**
"Velma! Velma! Njoo hapa. Kesho nitakutuma sokoni ukanunue mboga," Angelica alisema.

**(m)** Tambua kielezi katika sentensi ifuatayo **(alama1)**
Mwanafunzi yule mtiifu angalabu huwapendeza walimu wake.

**(n)** Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo:

**(i)** Chepchumba alikuwa anasoma darasani.
(Geuza kitenzi kisaidizi kuwa kitenzi kishirikishi) **(alama2)**

**(ii)** Roby alijitahidi sana.
Roby hakushinda mbio hizo.
(Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neno japo) **(alama2)**

**(o)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alama3)**
Mzee kijana aliyenunua gari juzi ametembelewa na wageni.

**(p)** Unaporidhika na jambo unasema ____________**,** unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi unasema _________na unapotaka usikivu unasema jamani/aisee **(alama2)**

**(q)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(alama1)**
KN (~~©~~) + KT (TS + T)

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 003

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Taja sifa za sauti zilizounda maneno yafuatayo **(alama2)**
**(i)** Paka
**(ii)** Chura

**(b)** Andika muundo wa silabi ya kwanza katika maneno yafuatayo: **(alama2)**
**(i)** Mwaga
**(ii)** Ng'ombe
**(iii)** Nzi
**(iv)** Kalamu

**(c)** Eleza matumizi ya kwa katika sentensi zifuatazo: **(alama2)**
**(i)** Wanangu walienda kwa ami yao
**(ii)** Wafanyakazi watatu kwa watano hujiuzulu kila mwezi

**(d)** Pigia mstari silabi inayotiliwa shadda katika maneno yafuatayo **(alama2)**
**(i)** Halafu
**(ii)** Rekebisha

**(e)** Andika sentensi ifuatayo katika wingi **(alama2)**

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na Imani.

**(f)** Ainisha vipashio vya kisarufi katika neno lifuatalo **(alama3)**

Hamkuwaona

**(g)** Bainisha viunganishi katika sentensi zifuatazo kisha uandike aina za viunganishi ulivyotambua **(alama2)**

**(i)** Zainabu alikuwa maskini licha ya kuwa mwimbaji hodari.
**(ii)** Kama unataka kufaulu soma kwa bidii

**(h)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**
**(i)** Mjohoro
**(ii)** Shajara

**(i)** Tunga sentensi ukitumia vivumishi vyenye dhana zifuatazo: **(alama3)**

**(i)** Kivumishi cha jina

**(ii)** Kivumishi cha pekee chenye dhana ya nyongeza

**(iii)** Kivumishi cha a – unganifu ngeli ya U – ZI

**(j)** Geuza sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama3)**
"Matokeo ya mtihani yanafurahisha," mwalimu mkuu akasema.

**(k)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana maagizo:

**(i)** Jamii yetu imeingiliwa na utamaduni wa kigeni

Bado tumehifadhi utamaduni wa kijadi.

(Unganisha kuwa sentensi ambatano) **(alama2)**

**(ii)** Sheria mpya inasema kwamba uuzaji wa nguo mpya umekubaliwa.
(Andika upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa kinyume) **(alama2)**

**(l)** Tunga sentensi zinazoonyesha majukumu yafuatayo ya vishazi vitegemezi **(alama2)**
**(i)** Kishazi kitegemezi cha sababu
**(ii)** Kishazi kitegemezi kirejeshi (kivumishi)

**(m)** Changanua sentensi ifuatayo kwa matumzi ya mishale **(alama4)**
Kinyang'anyiro hicho kilikamilika ulipokuwa Marekani.

**(n)** Andika ukubwa ukizingatia maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**
**(i)** Kidoo hiki hakifai, nunua kingine
**(ii)** Alijirembesha uso kwa poda

**(o)** Ainisha sentensi ifuatayo kidhamira na kimuundo **(alama2)**
Kikwai amemlaumu Mama Mercy ilhali kosa lilikuwa la Bosi.

**(p)** Bainisha maana mbili za sentensi zifuatazo **(alama2)**
**(i)** Bore alisema atakuja kesho
Yeye mwenyewe (Bore) atakuja.
**(ii)** Nitaweza kuwatembelea

**(q)** Tambua yambwa tendewa katika sentensi ifuatayo **(alama1)**
Mlinda lango alitupiwa mpira.

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 004

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**1. MATUMIZI YA LUGHA** **(alama40)**

**(a)** Tambulisha konsonanti katika maneno yafuatayo kisha utaje sifa tatu za kila mojawapo **(alama2)**

**(i)** Amani
**(ii)** Ruka

**(b)** Eleza tofauti kati ya sauti mwambatano na silabi mwambatano **(alama2)**

**(c)** Andika muundo wa silabi kwenye kiima katika sentensi ifuatayo **(alama1)**
Daktari amewasili hospitalini.

**(d)** Andika sentensi ifuatayo kwa wingi **(alama2)**
Kanga ya mwanamke huyo imerambwa vyema.

**(e)** Dhihirisha panapotiwa shadda katika kutamka maneno yafuatayo **(alama2)**
**(i)** Teketeza
**(ii)** Ukulima

**(f)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo **(alama2)**
Kiambishi awali cha ngeli, kiambishi cha wakati uliopita, kirejeshi ngeli ya KI – VI umoja, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda

**(g)** Unda nomino kutokana na vivumishi vifuatavyo; **(alama2)**
**(i)** Laghai
**(ii)** Tukutu

**(h)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**
**(i)** Veranda
**(ii)** Wakala

**(i)** Bainisha vielezi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani **(alama2)**
**(i)** Mtihani unatarajiwa kukamilika mapema.
**(ii)** Usalama wa Kijiji hiki umehimizwa mara kwa mara.

**(j)** Tunga sentensi yenye miundo ifuatayo **(alama2)**

**(k)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama3)**
"Huna budi kuandika kwa hati nadhifu" mwalimu akamsisitizia mwanafunzi.

**(l)** Changanua sentensi ifuatayo kwa matumizi jedwali **(alama4)**
Mti huo mzuri umeanguka.

**(m)** Tunga sentensi ukitumia kivumishi vifuatavyo **(alama3)**
**(i)** Kivumishi cha pekee (bila kubagua)
**(ii)** Kivumishi kimilikishi
**(iii)** Kivumishi cha jina

**(n)** Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Mwalimu alimnunulia mwanafunzi mrefu vitabu vitatu.

**(o)** Eleza matumizi ya kiambishi 'ka' na 'po' katika sentensi zifuatazo **(alama2)**

**(i)** Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani, akaoga.

**(ii)** Alipokwenda hapakuwa na ufanisi.

**(p)** Andika katika ukubwa ukizingatia maneno yaliyopigiwa mstari **(alama2)**

**(i)** Nguo zake zimelowa maji.

**(ii)** Njia hii imejaa vichochoro

**(q)** Ainisha kirai katika sentensi ifuatayo **(alama3)**

Kitabu hiki kizuri kinasomwa na watu wengi.

**(r)** Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi **(alama1)**

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 005

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** **(i)** Eleza tofauti iliyoko baina ya vipasuo vya kaakaa laini **(alama1)**

**(ii)** Andika sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye kaakaa gumu **(alama1)**

**(b)** Andika maneno mawili yenye silabi funge ambayo ni konsonanti pekee **(alama2)**

**(c)** Onyesha panapotokea shadda katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Kitabu

**(ii)** Barabara(baraste)

**(d)** Weka nomino zifutazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**

**(i)** Ndoo

**(ii)** Kucheka

**(e)** Ainisha vipashio vya kisarufi katika neno lifuatalo **(alama3)**

Hatukumpiga

**(f)** Kanusha sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Wewe umemaliza kulima shamba ambalo lingakuwa langu ningalifurahi.

**(g)** Tunga sentensi kinachodhihirisha matumizi ya vielezi vifuatavyo **(alama2)**

**(i)** Kielezi cha namna kiigizi

**(ii)** Kielezi cha namna kikariri.

**(h)** Andika sentensi ifuatayo kwa umoja **(alama2)**

Madomo ya madege yanaitwa majidona.

**(i)** Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:

**(i)** Chemutai amemlimia Kemunto shamba.
Kemunto amemlimia Chemutai shamba.
(Unganisha sentensi hizi bila kurudia kitenzi) **(alama2)**

**(ii)** Mwalimu huwafunza wanafunzi kwa ustadi mkubwa.
(Geuza katika wakati ujao hali timilifu) **(alama1)**

**(iii)** Nimemleta paka ili aue panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani
(Anza kwa: Panya) **(alama2)**

**(j)** Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vya pekee kudhihirisha maana ya: **(alama3)**

**(i)** Kutobagua

**(ii)** Kusisitiza

**(iii)** Kutobakisha ~ ngeli ya KI – VI umoja

**(k)** Geuza senntensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama2)**
“Tutafanya mtihani wa insha kesho,” wanafunzi walisema.

**(l)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(alama2)**

**(m)** Andika sentensi kubainisha aina zifuatazo za virai **(alama2)**

**(i)** Kirai tenzi kilicho na kitenzi kishirikishi kipungufu

**(ii)** Kirai kihusishi ambacho hufanya kama kiwakilishi.

**(n)** Bainisha matumizi ya ‘po’ katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Tulipowaona walikuwa wamesimama palipo na maegesho ya gari.

**(o)** Changanua sentensi ifuatayo kwa mstari **(alama2)**
Wale wengine watarudi kesho

**(p)** Andika sentensi upya ukianza kwa yambwa tendewa **(alama2)**
Velma amemjengea mama nyumba kwa matofali.

**(q)** Tunga sentensi ukitumia vihisishi vifuatavyo **(alama2)**

**(i)** Huruma

**(ii)** Kukataa

**(r)** Bainisha kiima na kiarifa katika sentensi ifuatayo **(alama1)**
Maji yote yaliyomwagika yalikuwa machafu.

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 006

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Linganisha na ulinganue sauti zifuatazo **(alama3)**
- **(i)** /th/ na /dh/
- **(ii)** /s/ na /z/
- **(iii)** /r/ na /l/

**(b)** Eleza maana ya silabi mwambatano **(alama1)**

**(c)** Andika muundo wa silabi ya kivumishi kwenye kiarifa katika sentensi ifuatayo: **(alama1)**
Mama mrefu anapika chakula kitamu.

**(d)** Andika vipashio vya kisarufi katika neno lifuatalo **(alama2)**
Sikumpigia

**(e)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**
- **(i)** Rinda
- **(ii)** Chandarua

**(f)** Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Uadilifu wa wafanyakazi hawa uliwapendeza wakurugenzi wa kampuni ya Darubini.

**(g)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja **(alama2)**
Walimu hawa walinunua nyuzi ambazo tutazitumia kushona.

**(h)** Onyesha panapotokea shadda katika maneno yafuatayo **(alama2)**
- **(i)** Ng'ombe
- **(ii)** Karatasi

**(i)** Ainisha uamilifu wa kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Kiatu cha mwalimu kimepatikana kando ya barabara.

**(j)** Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo:
- **(i)** Mwanafunzi ambaye hana kitabu hataweza kusoma.
  (Anza kwa: Kusoma...) **(alama2)**
- **(ii)** Magwasha alifiwa na mkewe.
  Mangwasha alimuoa Mirima
  (Unganisha ili kuunda sentensi changamano) **(alama2)**
- **(iii)** Wanafunzi hawa walikuwa wanacheza uwanjani
  (Badilisha kitenzi kisaidizi kuwa kitenzi kishirikishi kikamilifu) **(alama1)**

**(k)** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano **(alama3)**
- **(i)** La(tendeana)
- **(ii)** Vaa(tendwa)
- **(iii)** Nywa(tendeshwa)

**(l)** Tunga sentensi zenye vishazi vitegemezi vinavyoundwa kwa vipashio vifuatavyo **(alama3)**

**(i)** 'po' ya wakati

**(ii)** Kiunganishi cha sababu

**(iii)** Kirejeshi ambacho ni kiwakilishi katika ngeli ya A – WA

**(m)** Huku ukitoa mfano mwafaka, onyesha matumizi mawili ya ritifaa(') katika sarufi ya Kiswahili **(alama2)**

**(n)** Tunga sentensi ukitumia nomino ya kawaida wingi katika wakati ujao hali ya kuendelea **(alama1)**

**(o)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa **(alama2)**

Mwalimu: Kesho nataka uje ofisini mapema, unaskia?

Mwanafunzi: Bila shaka nitafanya hivyo.

**(p)** Dunisha sentensi ifuatayo **(alama1)**

Sahani zetu ziliznunuliwa bei ghali

**(q)** Changanua sentensi ifuatayo kwa matumizi ya jedwali **(alama3)**

Valeria na Valencia wanapika chakula kitamu.

**(r)** Ainisha yambwa katika katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Kashuu amemjengea mama yake mkubwa nyumbwa nzuri

**(s)** Tunga sentensi ukitumia aina zifuatazo za vihisishi **(alama2)**

**(i)** Mshangao

**(ii)** Kujuta

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 007

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Andika sauti mwambatano inayotamkwa kwenye: **(alama3)**
- **(i)** Kaakaa laini
- **(ii)** Midomo
- **(iii)** Midomo na meno

**(b)** **((i)** Ni nini maana ya silabi **(alama1)**
- **(ii)** Andika neno lenye silabi funge na silabi huru mbili **(alama1)**

**(c)** Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo **(alama2)**
- **(i)** Mke
- **(ii)** Mwanasheria

**(d)** Andika maneno yenye mofimu zifuatazo:
- **(i)** Nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendesha, kauli tenda. **(alama2)**
- **(ii)** Umoja (ngeli ya U- I) mzizi, kiishio **(alama1)**

**(e)** Andika viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo **(alama2)**
- **(i)** Mitume
- **(ii)** Kwetu

**(f)** Tunga sentensi yenye nomino ya wingi na kivumishi kiashiria cha mbali **(alama1)**

**(g)** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo:
- **(i)** Wesonga amempigia Bore simu.
  Bore amempigia Wesonga simu.
  (Unganisha sentensi hizi bila kurudia kitenzi) **(alama2)**
- **(ii)** Wafanyakazi wote watafanyiwa tathmini ili kupata suluhu ya matatizo hayo.
  (Badilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi) **(alama2)**
- **(iii)** Wanasayansi walifanya majaribio.
  Wanasayansi walipata tiba ya ugonjwa huo.
  (Tumia ka ya kuonyesha tukio moja ni matokeo ya tukio lingine) **(alama2)**
- **(iv)** Mabolezi walikuwa na majukumu makubwa.
  (Geuza katika umoja) **(alama1)**

**(h)** Andika sentensi ifutayo katika wakati uliopita hali ya mazoea **(alama2)**
Mwalimu atawaeleza wanafunzi kuhusu namna ya kuchanganua sentensi.

**(i)** Koloni/nukta mbili**(:),**hutumiwa katika kuorodhesha. Onyesha matumizi mengine matatu ya koloni **(alama3)**

**(j)** Andika sentensi ifutayo katika ukubwa **(alama2)**

Nyumba hizo zilijengwa mbali na mji ule.

**(k)** Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha **'a' unganifu** chenye dhana zifuatazo: **(alama3)**

**(i)** Uhusiano wa cheo

**(ii)** Nafasi katika orodha

**(iii)** Umilikaji

**(l)** Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa shamirisho kipozi **(alama2)**

Mfugaji aliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo.

**(m)** Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi kirejeshi kama: **(alama2)**

**(i)** Kiwakilishi

**(ii)** Kielezi

**(n)** Ainisha vielezi vya namna katika sentensi hii **(alama2)**

Mzee aliyevaa kinaijeria alitueleza kinagaubaga.

**(o)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(alama2)**

KN (N+V+E) + KT ($T_S$ + T +N+V)

**(p)** Ibadilishe chagizo ya mahali kuwa chagizo ya wakati **(alama1)**

Mutai aliucheza mpira mjini Nairobi.

**(q)** Tunga sentensi kuonyesha tofauti katika vitate vifuatavyo: **(alama1)**

Suka na zuka

# DARUBINI SERIES ~ 2026

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## JARIBIO LA 008

## 102/2 Kiswahili – Lugha ~ 2026 Muda: Saa 1

## MASWALI YA MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Taja sauti zenye sifa zifuatazo ukitumia neno: mbuzi **(alama2)**
- **(i)** Irabu ya nyuma, juu
- **(ii)** Sauti mwambatano ya midomoni
- **(iii)** Irabu ya mbele juu
- **(iv)** Kikwamizo ghuna cha masine

**(b)** Onyesha muundo wa silabi katika maneno yafutayo **(alama3)**
- **(i)** Mke
- **(ii)** Ng'ombe
- **(iii)** Ngoma

**(c)** Ainisha vipashio vya kisarufi (mofimu) katika maneno yafuatayo:
- **(i)** Ameteuliwa **(alama1)**
- **(ii)** Mtu **(alama1)**

**(d)** Weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka **(alama2)**
- **(i)** Mhindi
- **(ii)** Ukiritimba

**(e)** Tunga sentensi zifutazo **(alama2)**
- **(i)** ulizi
- **(ii)** ambatano

**(f)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Mpira ambao ni mpya umepotea.

**(g)** Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo **(alama2)**
Hildah alimpigia Eusebia mpira.

**(h)** Tambua aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo: **(alama2)**
Mzee huenda anacheza kamari.

**(i)** Andika kwa usemi wa taarifa: **(alama2)**
"Uchezeamo mna hatari," mama alinionya.

**(j)** Bainisha matumizi ya kiambishi 'kwa' katika sentensi zifuatazo **(alama2)**
- **(i)** Amepata alama kumi kwa ishirini
- **(ii)** Tutasafiri kwa kasi.

**(k)** Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine. **(alama1)**

**(l)** Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota(*) katika sarufi ya Kiswahili **(alama2)**

**(m)** Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali timilifu **(alama2)**

**(n)** Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi **(alama2)**

**(i)** Mwalimu mwenyewe aliendа shambani.

**(ii)** Kazi yetu haihitajika shuleni.

**(o)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama2)**

**(p)** Ainisha virai katika sentensi ifuatao **(alama2)**

Viongozi walikuwa waadilifu mno kabala ya uchaguzi.

**(q)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha visanduku **(alama4)**

Hili lake lilikuwa limeiva lakini hatukujua.

**(r)** Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee chenye dhana ya umilikaji **(alama1)**

**(s)** Bainisha kiima na kiarifa katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Wanafunzi waliotia bidii mwaka jana wamepita mtihani.

**(t)** Chakula ni kwa mlo, barabara ni kwa ……………………… na afya ni kwa……………………… **(alama1)**